JINA......................................NAMBARI.......................DARASA..............

102
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA
KISWAHILI
KIDATO CHA KWANZA
MACHI/ APRILI 2019

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA
HATI YA KUHITIMU KISOMO SNA SEKONDARI
KISWAHILI
MUDA: SAA 2 ½

## MAAGIZO

(i) Andika jina lako na nambari katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
(ii) Jibu maswali yote
(iii) Majibu yaandikwe katika nafasi ulizotengewa baada ya kila swali.
(iv) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(v) Kijikaratasi hiki kina kurasa saba zilizopigwa chapa.
(vi) Hakikisha maswali yote yapo.

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

Kwa matumizi ya mtahini pekee:

| SEHEMU | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| A. UFAHAMU | 15 | |
| B. SARUFI | 35 | |
| C. ISIMUJAMII | 10 | |
| D. FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA15)**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Mitandao ya kijamii ni mojawapo ya matokeo ya kuimarika kwa teknolojia ya mawasiliano. Baadhi ya mitandao ya kijamii ni **kitandazi** (facebook), twita na instagramu. Mitandao hii ya kijamii ina manufaa tele kama vile kuimarisha utangamano na kubadilisha mawazo baina ya walimu na wanafunzi kote duniani. Hata hivyo, mitandao ya kijamii ina madhara mengi hasa katika sekta ya elimu, si tu humu nchini bali ulimwenguni kote.

Mosi, viwango vya maadili shuleni hushuka kutokana na mitandao ya kijamii. Hii ni kutokana na baadhi ya picha na video zinazotazamwa katika mitandao ya kijamii. Baadhi ya picha na video huhusisha watu waliovua nguo na kusalia na suti ya Maulana kama walivyozaliwa. Wanafunzi na walimu wanaoyaenzi maadili **hawana budi** kuiambaa mitandao ya kijamii kiardhi na mbingu au mithili ya pepo mbaya.

Pili, mitandao ya kijamii imesababisha kuenea kwa matumizi ya dawa za kulevya. Baadhi ya video katika mitandao ya kijamii huhusisha watu wanaotumia dawa za kulevya; hasa nyimbo za kufokafoka. Lengo la baadhi ya video hizi ni kuwapotosha na kuwasawishi isivyo wanafunzi kwamba matumizi ya dawa za kulevya yana manufaa. Ni jambo la busara kujitenga nazo na kutoshawishika kuzitumia virahisi.

Tatu, mitandao ya kijamii huwapotezea wanafunzi muda wa kusoma, **kudurusu** na hata kufanya utafiti wa masomo yao. Hali hii husababisha matokeo duni katika mitihani. Ili kufua dafu masomoni, ni bora wanafunzi waipuzilie mbali mitandao ya kijamii.

Nne, fitina na uchochezi baina ya wanafunzi huweza **kusambazwa** na mitandao ya kijamii hasa kutokana na propaganda. Wanafunzi huchochewa kwa misingi ya dini na makabila wanayotoka. Aidha, baadhi ya migomo shuleni ina msingi wake kwenye mitandao ya kijamii pale ambapo shule moja inapogoma, nyingine hufuata mkondo. Ni muhimu kuepuka mitandao hii ili kutoathirika kihasi kwa wanafunzi.

Tano, mwingiliano na utangamano wa wanafunzi na wazazi wao **viamboni** huathirika kihasi na hata kufifia. Hii ni kwa sababu muda mwingi hutumiwa katika mitandao ya kijamii. Ni jambo lisilopingika kuwa muda mchache tu ndio unaotumiwa kutangamana na walio karibu. Ili kudumisha uhusiano mwema na wanaaila na majirani zetu, ni muhimu kujitenga na mitandao ya kutoathirika kihasi kwa wanafunzi.

Sita, vikundi vinavyoundwa kwenye mitandao ya kijamii ni vya kuwapotosha wanafunzi. Vikundi hivi hupigia ugaidi upatu, namna ya kukiuka sheria za shule miongoni mwa maovu mengine. Ni jambo la busara kwa mwanafunzi anayenuia kuwa mwongofu maishani kutojihusisha na vikundi hivi vya mitandao ya kijamii.

Saba, mitandao ya kijamii husifu vitendo vya kianasa. Baadhi ya picha ni za watu wanaopunga hewa na aghalabu huwa wanabugia vileo. Hili huwafanya wanafunzi kushawishika kujihusisha na anasa na upigaji mtindi. Wanapolewa chakari, fikra razini husambaratika hatimaye wengi wao hujihusisha na ukahaba na kuambukizwa magonjwa ya zinaa kama ukimwi. Hatima ya haya huwa ni kwenda waendako mahuluki wote.

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

Athari za mitandao ya kijamii zipo na pana haja ya mwanafunzi kugundua ukweli huu. Hili litawezesha wanafunzi kujitenga na mitandao hii wakiwa shuleni ili isiathiri masomo yao vibaya.

**Maswali**

(a) Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (alama1)

(b) Taja manufaa mawili ya mitandao ya kijamii kulingana na taarifa hii. (alama2)

(c) Je, kwa nini vikundi vinavyoundwa kwenye mitandao ya kijamii huwapotosha wanafunzi? (alama2)

(d) Kwa nini wanafunzi husawishika kupiga mtindi baada ya kuhusika na mitandao ya kijamii? (alama1)

(e) Eleza athari za kulewa chopi kwa wanafunzi. (alama3)

(f) Eleza madhara manne ya mitandao ya kijamii kwa mujibu wa kifungu hiki. (alama4)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(g) Eleza maana ya misamati ifuatayo kama ilivyotumika katika kifungu. (alama2)

(h) Kudurusu

(ii) viamboni

**SEHEMU YA B: SARUFI NA LUGHA**

(a) Eleza tofauti kati ya irabu na konsonanti. (alama2)

(b) Taja huku ukitoa mifano aina mbili kuu za ala za matamshi. (alama2)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(c) Taja njia mbili za kuainisha irabu. (alama2)

(d) Sauti [r] ni kimadende, [d] ni____________ ilhali [f] ni ________________ (alama2)

(e) Onyesha miundo ya silabi katika maneno yafuatayo. (alama2)

(i)Kichwa

(ii)Mbwa

(f) Kiimbo ni nini? (alama2)

(g) Weka shadda katika maneno yafuatayo ili kubainisha maana iliyo mabanoni.(alama2)
(i)Ala (kifaa)

(ii)Ala (mshangao)

(h) (i) Viambishi ni nini? (alama1)

(ii) Ainisha viambishi vyote katika neno lifuatalo. (alama3)
Watamsomea

(i) Kamilisha jedwali lifuatalo. (alama2)

| Kitenzi | Kutendwa | kutendea |
|---|---|---|
| (i)Lima | | Limia |
| (ii) Pika | | |
| (iii) Abudu | Abudiwa | |

(j) Ainisha maneno katika sentensi ifuatayo. (alama2)
Mchezaji hodari ameshinda tuzo.

(k) Taja matumizi yoyote mawili ya kikomo (.) (alama2)

(l) Tambua ngeli za nomino zifuatazo. (alama2)
(i)Mchuuzi

(ii)Asali

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(m) Andika upya sentensi ifuatayo katika wakati ujao. (alama2)
Wanafunzi wengi walifika shuleni jana.

(n) Badilisha sentensi ifuatayo katika hali timilifu (alama1)
Wazee wa kijiji wnataka kesi hii.

(o) Kanusha sentensi ifuatayo. (alama2)
Mzee analia shambani.

(p) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama2)
Maandishi yao ni mazuri sana.

(q) Eleza maana ya maneno yafuatayo. (alama2)
(i) Mkembe

(ii) Mkebe

**SEHEMU YA C: ISIMIU JAMII (ALAMA10)**

(a) Eleza maana ya isimu jamii. (alama2)

(b) Taja sifa zozote nne za lugha. (alama4)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(e) Nini umuhimu wa tanakali za sauti katika hadithi? (alama2)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(c) Taja umuhimu wa lugha katika jamii. (alama4)

**SEHEMU YA D: FASISIHI SIMULIZI (ALAMA20)**

(a) Eleza maana ya ngano (alama2)

(b) Taja sifa sita za ngano (alama6)

for more free revision content visit www.freekcsepastpapers.com

(c) Ni nini umuhimu wa fomula za kuanzia hadithi (alama4)

(d) Eleza umuhimu wa nyimbo katika hadithi (alama6)